

ASb  
approved



# Kisirusiru, Mjinga

Brigid Simiyu

Catherine Groenewald

Kiswahili





Hapo zamani za kale, kulikuwa na mkulima na mkewe.  
Walikuwa na mtoto mmoja pekee mvulana aliyetitwa  
Kisirusiru.




Kirusuru alipompeleka mbuzi malishoni, mbuzi alirarua shati lake. Mamake alimtuma sokoni kununua sindano aweze kushona shati lake. Kirusuru aliiweka sindano katika mfuko wa shati lake.



Njiani, Kisirusiru alijiunga na wavulana waliokuwa wakicheza mpira. Sindano ilipotea. Alipofika nyumbani, alisema, "Samahani mama, nimepoteza sindano njiani." "Mwanangu, wakati mwingine, idunge sindano kwenye karatasi kisha uiweke mfukoni," mamake alieleza. "Ndiyo mama, nimeelewa," Kisirusiru alijibu.

Kisirusiru alichukua chungu kwenda mtoni. Alikifungia chungu ndani ya kipande cha karatasi. Alipokuwa njiani, karatasi iliraruka, chungu kikaanguka chini na kuvunjika vigae vigae. Maji yote yalimwagika. Alipofika nyumbani, Kisirusiru alimweleza mamake, "Samahani mama, chungu kimeanguka na kuvunjika." "Mwanangu, wakati mwingine, kibebe chungu kichwani," mama alishauri. "Ndiyo mama, nimeelewa," Kisirusiru alijibu.





Siku iliyofuata, babake alimtuma Kisirusiru ampeleke mbuzi malishoni. Kisirusiru alimbeba mbuzi kichwani. Mbuzi alimpiga mateke na kumkwaruza kichwa hadi damu ikamtiririka usoni. Babake alikereka akamuuliza, "Utaacha ujinga wako lini? Mbuzi hufungwa na kuvutwa kwa kamba! Usipokuwa mwerevu, utalazimika kuhama hapa nyumbani."



Siku iliyofuata, babake alimtuma akanunue nyama sokoni.  
Kisirusiru alikumbuka alivyoambiwa na babake. Aliifunga  
nyama kwa kamba akaivuta kuelekea nyumbani. Alikimbia ili  
babake asisubiri kwa muda mrefu. Hebu fikiria, nyama hiyo  
ilikuwaje alipowasili nyumbani?





Babake alikasirika mno akamwambia afunganye virago vyake ahame nyumbani. Mamake aliposikia hivyo, aliamua kuondoka pamoja na mtoto wake. Waliung'oa mlango wa jikoni wakaubeba ili wawe na kitu cha kuanzia ujenzi wa nyumba yao mpya.



Walitembea kwa muda mrefu. Lakini, hawakufanikiwa kupata mahali pa kujenga nyumba yao mpya. Giza lilipoingia, waliamua kukwea mti na kulala pale.



Kisirusiru na mamake waliamua kuanza kukaa juu ya mti. Walikuwa wakiuvuta mlango juu waliposikia makelele chini. Walipotazama chini, waliwaona wavulana watatu waliobeba magunia makubwa. Waliogopa sana wakauachilia mlango ukaanguka kwa kishindo. Kishindo cha mlango kiliwaogofya wavulana wale watatu wakaacha kila kitu na kutoroka.



Kisirusiru na mamake walishuka chini, wakayafungua yale magunia. Humo walipata pesa, nguo, mablanketi, na kila kitu walichohitaji kuanzisha nyumba yao. Punde, walipata pahali pa kujenga nyumba. Waliishi kwa furaha tangu siku hiyo.

You are free to download, copy, translate or adapt this story  
and use the illustrations as long as you attribute in the  
following way: Cissy Kiwanuka Luyiga Author - Cissy

Kiwanuka Luyiga

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Catherine Groenewald

Language - Kiswahili

Level - Longer paragraphs © African Storybook Initiative

2014

Creative Commons: Attribution 3.0

Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)



